

TANGAZO MUHIMU

Mpendwa Mteja,

Benki kuu ya Tanzania (**BOT**) imezielekeza benki zote kuboresha baadhi ya taarifa za wateja, lengo la zoezi hili ni kuweze ha benki kuwa na taarifa sahihi na zenye uhakika za wateja.

Kutokana na zoezi hilo wateja wote wanatakiwa kuwasilisha barua ya utambulisho iliyosainiwa kutoka Ofisa Mtendaji wa kijiji, Ofisa Mtendaji wa kata au Mwajiri, Barua hiyo inatakiwa kuwa na taarifa zifuatazo:

- Tarehe ya Kuzaliwa
- Mahali ulikozaliwa
- Sehemu/ mahali unapotokea na anuani yako ya sasa
- Makazi yako ya sasa (Mtaa/kijiji/ mji/ jiji/ wilaya) pamoja na vitu muhimu vilivyo karibu na mahala anapoishi mteja.
- Nambari ya simu yako ya mkononi
- Anuani ya barua pepe (e-mail)(kama ipo)
- Kwa muda gani umekuwa ukiishi katika makazi yako ya sasa
- Picha ya pasipoti

Kutokana na maelekezo ya BOT zoezi hili litahusisha wateja wote waliopo na wale wapya . Na zoezi lenyewe litaanza **Novemba 21, 2011** hadi **Machi 31, 2012**.

Tafadhali fika katika tawi lolote la NMB na wasiliana na dawati la huduma kwa wateja kwa ajili ya kuchukua fomu zinazotakiwa kujazwa. Baada ya kujaza fomu hizo, tafadhali zirejeshe katika dawati la huduma kwa wateja kwenye tawi lolote la NMB lililo jirani ukiambatania na nyaraka zote zinazotakiwa.

Asante kwa ushirikiano wako wa siku zote